## HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MENEJIMENTI ROBO YA TATU KILICHOFANYIKA TAREHE 08/04/2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

### WATENDAJI WALIOHUDHURIA:

1. Ndg. Leokadia Humera - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji(W)
2. Ndg. Said I. Ally - Afisa Utumishi (W)
3. Ndg. Beatrice Balige - Kaimu Afisa Elimu (W)
4. Dr. Chrispin Shami - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
5. Ndg. Wiltihelimma Nkunga - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W)
6. Dr. John Nyorobi - Kaimu Mganga Mkuu (W)
7. Ndg. Khadija M. Kwikima - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika (W)
8. Ndg. Benjamini Sarakikya - Kaimu Mhandisi Ujenzi (W)
9. Ndg. Dorcas P. Ningha - Kaimu Mkuu Kitengo cha Nyuki (W)
10. Ndg. Majura - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
11. Ndg. Thomas Lutego - Afisa Habari
12. Ndg. Peniel J. Titus - Afisa Mipango (W)
13. Ndg. Joseph Yamo - Afisa Ugavi
14. Ndg.Jonas Sindaguru - Kaimu Mkuu Ukaguzi wa Ndani (W)
15. Ndg. Luko Mtekozn - Kitengo cha TEHAMA (W)
16. Ndg. Juliana Luhasile - Kaimu Mkuu Kitengo cha Uvuvi (W)
17. Ndg. Perpetua Chonja - Afisa Tarafa Usagara
18. Ndg. Peter Michael - Afisa Tarafa Misungwi
19. Ndg. Cresensia Mwalongo - Afisa Tarafa Mbarika
20. Ndg. Gloria Kaywanga - Afisa Tarafa Inonelwa
21. Ndg. Gloria Buname - Mratibu wa TASAF
22. Ndg. Felix Safan - Afisa Mapato
23. Ndg. Faustini Salala - Mthibiti Ubora wa Shule (W)
24. Ndg. Steven Singira - Mkuu wa Kitengo cha Sheria (W)
25. Ndg. Stella Musangya - Mweka Hazina (W)
26. Ndg. Manyanza Mageme - Kaimu Katibu TSC
27. Ndg. Renatus Nyasebwa - Kaimu Afisa Ardhi (W)
28. Ndg. Musa - Kaimu Afisa Mazingira (W)

### SEKRETARIETI

1. Ndg. Jackson J. Igenge
2. Ndg. Restuta Pamba
3. Ndg. Bruno Simon
4. Ndg. Martha Mbise

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufunga kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha mihtasari wakikao cha Menejimenti cha tarehe 17/3/2022 na 18/3/2022
4. Yatokanayo
5. Kupitia muhtasari wa kamati ya robo ya pili 2021/2022
    a) Muhtasari wa kamati ya Udhibiti Ukimwi wa tarehe 14/2/2022
    b) Muhtasari wa kamati wa Huduma Za Kijamii wa tarehe 15/2/2022
    c) Muhtasari wa kamati ya Huduma za kiuchumi wa tarehe 16/2/2022
    d) Muhtasari wa Baraza la Madiwani kawaida wa tarehe 10-11/3/2022
    e) Muhtasari wa kamati ya Fedha, uongozi na mipango tarehe 31/3/2022

6. Taarifa ya mapato na matumizi kuishia mwezi Marchi 2022
7. Taarifa ya shughuli za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha robo ya tatu 2021/2022.

8. Taarifa za Kisekta
    i. Utawala na Rasilimali watu
    ii. Elimu Sekondari
    iii. Elimu Msingi
    iv. Ardhi na Maliasili
    v. Mifugo na Uvuvi
    vi. Maendeleo ya Jamii
    vii. Usafi na Mazingira
    viii. Manunuzi
    ix. TEHAMA
    x. Sheria
    xi. Uthibiti Ubora wa Shule
    xii. Nyuki
    xiii. Afya
    xiv. Kilimo na Ushirika

9. Muundo na mgawanyo wa majukumu katika Serikali za Mitaa (MSM).
10. Taarifa za utekelezaji wa zoezi la anuwani za makazi na postkodi.
11. Mapendekezo ya vyanzo vya mapato vitakavyo kusanywa na Mamlaka katika mwaka wa fedha 2022/2023
12. Taarifa ya mapokeo ya fedha kiasi cha Tsh 456,505,242.42 kwa ajili ya Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mwanangwa.
13. Taarifa ya mkataba wa malipo ya madini ya ujenzi baina ya Halmashauri ya wilaya ya Misungwi na kampuni ya China Civil Engineering Contruction Corporation (CCECC) mradi wa ujenzi wa reli ya SGR.
14. Kufunga kikao

**MUHT. NA. 53/4/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe kwenye kikao na kuwaomba kushiriki kikamilifu katika kujadili agenda zilizokuwa mezani kisha alifungua kikao saa 3:25 Asubuhi.

**MUHT. NA. 54/4/2022: KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu wa kikao aliwasilisha agenda 14 zilizokuwa mezani, wajumbe walizipokea na kukubaliana ziweze kujadiliwa kisha kikao kiliendelea.

**MUHT. NA. 55/4/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MENEJIMENTI WA TAREHE 17/03/2022 NA 18/03/2022:**

Mihtasari iliwasilishwa mbele ya wajumbe, waliipokea na kuipitia ukurasa kwa ukurasa na kithibitisha kuwa ni sahihi kasha Katibu na Mwenyekiti waliisaini kuwa kumbukumbu sahihi ya Kikao.

**MUHT. NA. 56/4/2022 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/3/2022:**

Utekelezaji wa maazimio yaliyokuwa yametolewa yaliwasilishwa kama ifuatavyo;
Kuhusu azimio la kufanya ufuataliaji wa mapato yatokanayo na tozo za taka ngumu katika kampuni ya wachina SGR kata ya Fela ufanyike. Ilielezwa kuwa utekelezaji unaendelea ambapo taratibu za uandaaji wa mkataba zinaendelea

Kuhusu azimio la kuwapaitia Wakuu wa Idara na Vitengo wapatiwe muundo mpya uliotolewa kwenye uandishi wa barua za Ofisi,Utekelezaji ulifanyika na muundo huo ulitolewa.

Kuhusu azimio la kufanya Ufuatiliaji ili kujua kiasi cha fedha za CHF wanachotakiwa kutoa wanafunzi wa Sekondari na taarifa iwasilishwe kwenye kikao. Iliezezwa kuwa kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa wanafunzi ni Tsh. 30,000/= kwa mwaka kwa watu wasiopungua sita kwa kila kaya.

Kuhusu azimio la kuwasilisha taarifa ya fedha za Jengo la Halmashauri zilizotumika kwa kipindi cha mwezi Januari 2022 kulipa TBA. Ilielezwa kuwa fedha iliyolipwa kwa Mkandarasi wa Jengo la Halmashauri (TBA) kwa kipindi cha mwezi Januari 2022 ni Tshs. 71,000,000/=.

**MUHT. NA. 57/4/2022 KUPITIA MIHTASARI YA VIKAO CHA KAMATI NA BARAZA ROBO YA PILI:**

Wajumbe walipitia mihtasari pamoja na maazimio ya vikao vya robo ya pili na kuchangia ambapo walifanya marekebisho yaliyoonekana na kupitia kusisitiza maazimio yote yaliyotolewa yafanyike kwa usahihi na kwa yale yanayohitaji viambata, viwasilsihwe Ofisi ya Katibu wa vikao ili viambatanishwe kwenye kabrasha.

**MUHT. NA. 58/04/2022 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA MWEZI MACHI 2022:**

Taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kuishia Mwezi Machi 2022 kama ifuatavyo:-

Mapato kutokana na vyanzo vya ndani (Own source)Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha Tshs. 2,523,951,580.00 ikiwa ni lengo la mwaka mzima kama ruzuku ya matumizi mengineyo hadi kufikia mwezi. Hadi kufikia mwezi Machi 2022 jumla ya Tshs. 1,803,249,490.01 sawa na asilimia 71.45 ya lengo la mwaka zilikuwa zimekusanywa ambapo kwa mwezi Machi pekee kiasi cha Tsh. 241,601,005.89 kilikusanywa .

Kwa upande wa matumizi , Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilikisia kutumia kiasi cha Tsh. 61,118,705,810.04 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia mwezi Machi,2022 kiasi cha Tsh. 6,658,553,989.72 sawa na asilimia 48.2 kilikuwa kimetumika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kufanya majadiliano kama ifuatavyo;

Wajumbe walishauri vyonzo vyote vilivyopo chini ya asilimia 70 ya lengo la mwaka mzima 2022 vifuatiliwe ikiwa ni pamoja na Leseni za vileo,pikipiki, faini mbalimbali, Ada za zabuni, Ada ya Michezo ili kufikia lengo.

**AZIMIO.**

Ufanyike ufuatiliaji wa mapato fungiwa ya CHF ya mwezi Januari hadi Machi 2022.

**MUHT. NA. 59/4/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KIPINDI CHA ROBO YA TATU 2021/2022**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya tatu kuishia mwezi Machi 2022 kwa mchanganuo ufuatao:-

| Na | Jina la Mradi | Fedha pangwa | Fedha tolewa | Fedha tumika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Miradi ya Mapato ya Ndani (40%) | 713,608,632.00 | 448,918,824.00 | 176,406,975.00 |
| 2. | Mfuko wa Jimbo (CDCF) | 67,524,000.00 | 67,524,000.00 | 0 |
| 3. | Ukamilishaji wa Jengo la Ofisi za Halmashauri- Serikali kuu | 500,000,000.00 | 500,000,000.00 | 0 |
| 4. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati 3 - Serikali kuu | 150,000,000.00 | 150,000,000.00 | 85,309,200.00 |
| 5. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya - Serikali kuu | 800,000,000.00 | 800,000,000.00 | 0 |
| 6. | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 09 vya madarasa katika Shule za Msingi - Serikali kuu | 112,500,000.00 | 112,500,000.00 | 92,820,500.00 |

| Na | Jina la Mradi | Fedha pangwa | Fedha tolewa | Fedha tumika |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 09 vya madarasa katika Shule za Sekondari– Serikali kuu | 112,500,000.00 | 112,500,000.00 | 76,472,500.00 |
| 8. | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 07 vya maabara katika Shule za Sekondari 3 – Serikali kuu | 150,000,000.00 | 150,000,000.00 | 61,500,000.00 |
| 9. | EP4R – Msingi | 321,581,500.00 | 0 | 0 |
| 10. | EP4R – Sekondari | 346,581,500.00 | 0 | 0 |
| 11. | SEQUIP – Ujenzi wa S/Sekondari Manawa | 1,075,200,000.00 | 470,000,000.00 | 71,841,700.00 |
| 12. | LANES – Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na choo matundu 6 S/Msingi Sanjo | 64,510,000.00 | 46,600,000.00 | 31,121,900.00 |
| 13. | Benki ya Dunia - (SWASH) | 300,000,000.00 | 0 | 0 |
| 14. | TAHEA | 60,000,000.00 | 0 | 0 |
| 15. | Global Fund | 62,986,000.00 | 8,511,965.76 | 4,818,479.53 |
| 16. | Negleted Tropical Diseases – NTD | 23,329,000.00 | 0 | 0 |
| 17. | AGPAH/Amref | 176,280,000.00 | 34,880,000.00 | 32,900,000.00 |
| 18. | U5BR – Child Survival/ UNICEF | 10,000,000.00 | 5,000,000.00 | 0 |
| 19. | Health Sector Basket Fund – HSBF | 802,861,000.00 | 309,014,958.83 | 174,579,069.7 |
| 20. | TASAF | 9,317,649,000.00 | 2,098,144,945.00 | 2,005,183,530.00 |
| 21. | Elimu Bila malipo – Msingi | 1,285,509,000.00 | 815,232,248.84 | 815,232,248.84 |
| 22. | Elimu Bila malipo – Sekondari | 717,855,000.00 | 427,998,151.72 | 427,998,151.72 |
| 23. | Fedha za Mitihani – Msingi | 424,905,500.00 | 424,905,500.00 | 424,905,500.00 |
| 24. | Fedha za Mitihani – Sekondari | 358,761,500.00 | 358,761,500.00 | 337,145,000.00 |
| | **Jumla Kuu** | **17,954,141,632.00** | **7,340,492,094.15** | **4,818,234,754.79** |

Aidha aliwasilisha Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa nje ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo:-

| Na | Jina la Mradi | Fedha tolewa | Fedha tumika |
|---|---|---|---|
| 1. | SERIKALI KUU (TOZO) - Ujenzi wa kituo cha Afya Usagara na ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa S/Sekondari Kanyelele na Mamaye | 550,000,000.00 | 278,019,673.38 |
| 2. | EP4R - (Ujenzi wa vyoo matundu 12 S/Msingi Isuka na Igenge) | 13,200,000.00 | 10,839,200.00 |
| 3. | SWASH - Ujenzi wa matundu 66 ya vyoo S/Msingi Busegeja, Mapilinga na Mwajombo | 85,317,250.56 | 81,382,900.00 |
| 4. | Uhamasishaji na utoaji wa chanjo ya UVIKO -19 - Awamu ya kwanza | 57,888,303.59 | 57,888,303.59 |
| 5. | Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 (IFM) - Ujenzi wa vyumba 146 vya madarasa katika Shule 32 za Sekondari na nyumba moja ya watumishi wa Afya Mwawile Zahanati (3 in 1) | 3,016,514,747.00 | 2,859,560,848.40 |
| 6. | WASH - Ujenzi wa Matundu 35 ya vyoo, ujenzi wa mfumo wa kuvunia maji ya mvua na ularabati wa vyumba 15 vya kujifungulia katika Zahanati 15 | 475,715,000.00 | 74,061,900.00 |
| 7. | RBF - Mpango wa Malipo kwa Ufanisi | 25,068,982.86 | 10,547,459.27 |
| 8. | Uhamasishaji na utoaji wa chanjo ya UVIKO -19 - Awamu ya pili | 20,217,391.30 | 20,217,391.3 |
| 9. | UVIKO - 19 - Uwekaji wa Mfumo wa Maji, vifaa vya kunawia mikono, uvunaji wa maji ya mvua/uunganishaji ya maji ya bomba/uchimbaji wa visima katika Shule ya Msingi Chatta na Iteja na S/Sekondari Nhundulu | 35,617,139.58 | 29,978,281.70 |
| 10. | Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 (IFM) - Mishahara ya watumishi 2 wa muda wa Afya | 8,675,960.00 | 0 |
| | **Jumla Kuu** | **4,288,214,774.89** | **3,422,495,957.64** |

Vilevile aliwasilisha taarifa ya Fedha za bakaa 2020/2021 kuishia 31, Disemba, 2021 kwa mchanganuo ufuatao:-

| Na | Jina La Mradi | Fedha Iliyokuwa Imebaki | Fedha Tumika |
|---|---|---|---|
| 1. | Ukamilishaji wa Jengo la Halmashauri | 106,706,650.57 | 71,000,000.00 |
| 2. | Uendelezaji wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya - Iteja | 868,183,630.02 | 727,183,630.32 |
| 3. | Mfuko wa Afya ya Pamoja (HSBF) | 267,954,024.93 | 267,954,024.93 |
| 4. | Mpango wa Malipo kwa Ufanisi - RBF | 79,573,300.59 | 77,638,641.59 |
| 5. | Uchangiaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Mapato ya ndani | 84,000,000.00 | 82,572,584.00 |
| | **Jumla Kuu** | **1,429,945,607.09** | **1,226,348,880.84** |

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuchangia kama ifuatavyo Wajumbe walishauri Idara zenye fedha za bakaa zifanye ufuatiliaji ili zitumike kama zilivyokusudiwa. Miradi yote itembelewe na kusimamiwa kwa ushirikiano ili ikamilike kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa hasa miradi ya Afya na Elimu.

**MUHT. NA. 60/4/2022 TAARIFA ZA KISEKTA:**

Idara ziliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha robo ya tatu kama ifuatavyo:-

1. Idara ya Utawala na Rasilimali watu ilitekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupoke watumishi 2 wa Idara ya Afya kutoka OR – TAMISEMI ambapo ajira yao ilitokana na mradi wa COUP. Kuhamisha watumishi 20 kwenye mfumo

   walihama kutoka Halmashauri ya Misungwi kwenda Halmashauri zingine. Kupokea na kuwaingiza kwenye mfumo watumishi 4 walihamia Wilaya ya Misungwi kutoka Halmashauri zingine. Kuwaondoa kwenye mfumo watumishi 4 walistaafu Utumishi wa Umma.

2. Idara ya Elimu Msingi ilitekeleza shughuli za kusimamia zoezi la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza 2022,kufanya usajili wa wanafunzi wa darasa la IV na VII kwa ajili ya mtihani wa taifa 2022,kusimamia na kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji na utoaji mazoezi na majaribio yanayotolewa shuleni na pia kusimamia kufanyika kwa kikao cha wadau wa elimu Wilaya ya Misungwi.

3. Idara ya Elimu Sekondari, Kazi zilizofanyika ni pamoja na kusimamia ujenzi wa shule mpya za Sekondari kwa nguvu za wananchi,kupokea matokeo ya mitihani ya kidato cha nne 2021 ambapo ufaulu ulipanda toka asilimia 93.69 hadi 94.30, kutoa motisha kwa wlimu wa sekondari waliofaulisha kwa kiwango cha alama "A" kitado cha IV na VI na kuandikisha wanafunzi wa kidato cha kwanza 2022.

4. Idara ya ardhi na maliasili ilifanya shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa na kusambaza Ankara za malipo ya gharama za hati kwa wananchi,kutoa na kusambaza hati za madai kwa wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi na kuandaa michoro ya mipango miji kwa matumizi sahihi ya ardhi.

5. Idara ya mifugo na uvuvi ilitekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kwa upande wa Sekta ya Mifugo, shughuli za ugani zilifanyika katika kata zote 27 na vijiji 114 kupitia maafisa ugani 33 wa mifugo waliopo, wafugaji walielimishwa juu ya unenepeshaji wa mifugo,wafugaji/wadau wa mifugo walipata elimu ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa njia ya uvalishaji hereni.

Kwa Sekta ya Uvuvi iliendelea kusimamia sheria, Kanuni na taratibu zilizo katika Nyanja ya Ulinzi na usalama wa rasilimali za ziwa, ilifanya doria 3 za majini na kukamata zana za uvuvi haramu ikiwemo timba 5, nyavu za makila chini ya nchi sita 462, tupatupa 2, katuli 5 mitumbi 4 nyavu haramu zilihifadhiwa kwenye stoo za BMU ya Mwalogwabagole na Kigongo feri pia Elimu ya Uvuvi Endelevu na Lesseni za Uvuvi ilitolewa.

6. Idara ya maendeleo ya Jamii kazi zilizofanyika ni pamoja na ufuatiliaji wa marejesho kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu, kusajili vikundi na kutoa mafunzo ya utumiaji wa mikopo inayotolewa,kutoa elimu ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

7. Idara ya Uhifadhi wa mazingira na udhibiti takangumu ilifanya kazi mbalimbali zikiwemo,kuhamasisha jamii juu ya usafi wa Mazingira wa kila siku na Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi sambamba na uzoaji wa Taka tani 72 za kutupwa Dampo,kuhamasisha jamii, shule, Zahanati Vikundi na taasisi juu ya utekelezaji wa Kampeni ya usafi na upandaji Miti katika vijji vyote 115,kufanya ukaguzi wa Mazingira umefanyika katika viwanda 2, vituo vya mafut 2, karakana za kuchomelea vyuma na vioo na kushirikiana na TASAF kufanya tathimini ya mazingira na Kijamii kwa miradi 11 ya ujenzi wa Barabara za TASAF.

8. Kitengo cha manunuzi kilisimamia matumizi ya fedha kiasi cha Tshs. 303,491,747/= ambacho kilitumika kwa Idara zote kwa kipindi cha Mwezi Januari hadi Machi 2022.

9. Kitengo cha TEHAMA kilifanya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuratibu na kusimamia uingizaji wa taarifa za Anwani za Makazi na POSTIKODI katika mfumo na NAPA,kufanya matengenezo ya mashine 6 za kukusanyia mapato (POS),kusajili vyanzo vya mapato katika (POS)na kuratibu na kusimamia utengenezaji vitambulisho 188 vya watumishi wa idara mbalimbali.

10. Kitengo cha sheria kilifanya kazi za usimamizi wa mabaraza ya kata kwa kutoa maelekezo na usharui kwa wajumbe wa mabaraza hayo,kusimamia mashauri ya madai,kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo za Halmashauri na kuendelea

kutoa elimu na kufanya ufuatiliaji wa makosa ya jinai kwa wadaiwa wa ushuru wa huduma (servicely).

11. Idara ya afya ilitekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukusanya damu kiasi cha units 490,kutembelea vituo 15, kuhamasisha na kuboresha miundombinu ya WASH,kusimamia huduma na rufaa za watoto 3 wahanga wa ubakaji hospitali na polisi kwa maslahi mapana ya watoto,kuhakiki data zilizoingizwa kwenye mfumo wa DHIS2 kwa vituo vyote na kutoa mafunzo kazini juu ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwend kwa mtotot katika vituo 4 vya kutolea huduma ambavyo ni mwamazengo, mwagiligili, kaseni na mwaniko.

12. Idara ya uthibiti ubora wa shule ilifanya kazi za kuona ufundishaji na uwajibikaji wa walimu pamoja na ujifunzaji wa wanafunzi darasani,kuhimiza mahudhurio ya walimu na wanafunzi shuleni,kukutana na jamii inayozunguka shule hizo wakiwemo wawakilishi wa serikali ya Kijiji, Wazazi na Kamati ya shule na kufanya nao Kikao juu ya kuboresha shule zao,kukutana na wamiliki wa shule binafsi na kuwashauri juu ya ukamilishaji wa miundombinu ili shule hizo ziombewe kibali cha Bweni kuhimiza walimu ili wawasimamie wanafunzi kwa karibu Zaidi kwa lengo la kumudu stadi za kusoma kuandika na kuhesabu (KKK).

13. Kitengo cha nyuki kilifanya shughuli za kukagua ubora wa mizinga mipya kumi (10) kwa mfugaji mmoja aliyeko Usagara,kuweka mazingira salama kwa mtu mmoja wanaofuga nyuki, kukagua manzuki moja iliyopo kijijicha Nyamayinza na kuhamasisha vikundi vya vijana kufuga nyuki.

**MUHT. NA. 61/04/2022 MUUNDO NA MGAWANYO WA MAJUKUMU KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MSM)**

Muundo huo uliwasilishwa kwa wajumbe waliupokea bila hoja na agenda ilifungwa.

**MUHT. NA. 62/04/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTKODI WILAYA YA MISUNGWI:**

Taarifa hiyo iliwalishwa kwa wajumbe kwamba zoezi la kuingiza taarifa kwenye mfumo lilianza tarehe 1/4/2022 na jumla ya anwani 53,397 zilisajiliwa katika mfumo kufikia tarehe 12/4/2022 na zoezi linatarajiwa kukamilika tarehe 15/4/2022.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo bila hoja na agenda ilifuangwa.

**MUHT. NA. 63/04/2022 MAPENDEKEZO YA VYANZO VYA MAPATO VITAKAVYOKUSANYWA NA MAWAKALA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023:**

Mapendekezo hayo yaliwasilishwa ambapo wajumbe walipitia na kukubaliana na vyanzo vilivyopendekezwa vikusanywe na mawakala. Pia wajumbe walishauri agenda hiyo ipelekwe kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa maamuzi zaidi na agenda ilifungwa.

**MUHT. NA. 64/04/2022 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 456,505,242.42 KWA AJILI YA UJENZI WA SHULE YASEKONDARI YA WASICHANA MWANANGWA:**

Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa wajumbe na ilipokelewa bila hoja na agenda ilifungwa.

**MUHT. NA. 65/04/2022 TAARIFA YA MKATABA WA MALIPO YA MADINI YA UJENZI BAINA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI NA KAMPUNI YA CHINA CIVIL ENGINEERING CONTRUCTION CORPORATION (CCECC) MRADI WA UJENZI WA RELI YA SGR.**

Taarifa iliwasilisha kwamba Kampuni za CCECC na CCRC zinazofanya Ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa SGR (Isaka – Mwanza) zilionesha kutoridhika na makubaliano yaliyofikiwa awali kuwataka kulipa ushuru wa madini ujenzi kwa kiwango cha Bilioni mbili na milioni miatano (2.5bil) kwa kipindi cha miaka mitatu.

Walisema sababu kuu iliyosababisha kukataa ilikuwa kiwango cha fedha kilichopangwa hakikukidhi hali halisi ya madini ujenzi ambayo yatahitajika katika mradi kwa mujibu wa mpango wa mradi.

Kampuni zilieleza kuwa kuna marekebisho ya mpango wa mradi ambapo yamepunguza ukubwa wa mradi hivyo kuathiri mahitaji ya madini ya ujenzi. Hivyo Kampuni zilikubali kulipa ushuru wa madini ya ujenzi jumla ya kiwango cha Tshs.

946,005,062.60/= ambapo waliomba kulipa kila baada ya miezi 3 kiasi cha Tshs. 78,833,755.22/= kwa Halmashauri.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe walichangia kama ifuatavyo;

Wajumbe walikubaliana Kampuni ilipe kiasi hicho na endapo kiasi cha madini ujenzi kitaongezeka wataongeza ushuru kulingana na madini ujenzi yatakayoongezeka.

Pia Mwanasheria ahakikishe mikataba inawekwa vizuri ili ufuatiliaji uwe rahisi.

**MUHT. NA. 66/04/2022 KUFUNGUA KIKAO:**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe pamoja na wataalamu kwa ushiriki wao katika agenda zilikuwa mezaji na kasha alifunga Kikao saa 12:46 jion.

.........................................
SAINI YA KATIBU WA KIKAO

.........................................
SAINI YA MWEMYEKITI WA KIKAO

TAREHE YA KUTHIBITISHWA MUHTASARI......24/05/2022......